AckySHINE.com

# Kanuni ya fedha ya matumizi na mipango ambayo itakusaidia ukiifuata

By SW - Melkisedeck Shine · June 10, 2021

Biashara - Mbinu za Ujasiriamali na Biashara Kufanya tofauti · #Karibu AckySHINE · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF · #Ujasiriamali: Matumizi ya Fedha

Jifunze kanuni za fedha kama ilivyoainishwa hapo chini. Fedha inatakiwa uwe na nidhamu nayo katika kutumia Hii kanuni inatumika kwenye vyanzo vyako vyote vya fedha ili uwe na mafanikio yenye amani

Tuangalie hapa chini hizi kanuni???

Fungu la kumi 10% Akiba 30% Matumizi 40% Dharura 10% Msaada 5% Sadaka 5%

??hii kanuni inafanya kazi katika kila hela unayopata kama faida

Mfano : mtu mwenye mshahara wa mil 1 unayoipata kila mwezi baada ya makato

Fungu la kumi 10% (Tithe) hii ni mali ya Mungu si yako!!

?itakuwa ni sh laki 1 unatakiwa uitoe sehemu unayoabudia kila mwezi na kama unabiashara zako faida yake ndani yake toa fungu la kumi Pia hata kama ni hela unapewa kama zawadi itolee fungu la kumi

?faida ya hii

?inalinda kazi au Biashara unayoifanya zidi ya adui ?magonjwa,ajali , ( vitu vitakavyokufanya utumie hela bila mpangilio),etc yanakuwa mbali nawe

Akiba 30%

?hii unaiweka kwa matumizi yako ya baadae kama kujenga,kusomesha,kulima, investment, etc ?unatenga laki 3 kwa mtu anaepokea mil 1

Matumizi 40%

?hii itatumika kwa matumizi ya kila siku ,chakula ,Maji, etc

?hapa unatenga laki 4 kwa ajili ya matumizi kwa mtu wa mshahara wa mil 1 ?note : hapa ndio hela yako ya kustarehe inatoka Angalia matumizi yasizidi hela uliyonayo ?wengi wao hapa watu ndio inamfanya awe na vyanzo vingi vya hela ili aweze kufanya starehe awezavyo ?pia hii ndio hela unayotoa kwa ajili ya mbegu (sadaka ya gharama) wanaoifahamu

Dharura 10%

?hii fedha unaitunza kwa ajili ya vitu usivyotarajia kama msiba, ndugu kuumwa au kukwama etc ?unatunza laki 1 kwa mtu wa mshahara wa mil 1

Msaada 5%

?hii inawahusu watoto yatima, wajane na wasiojiweza kama vilema ?unatoa elfu 50 kwa mtu wa mshahara wa mil 1 ?unaigawa kama unamagroup yote hayo

Sadaka 5%

?hii unatoa elfu 50 kwa mtu wa mshahara wa mil 1 ?igawe mara NNE coz mwezi una jumapili 4 ambayo utapata ni elfu 12500 ivyo basi kila jumapili peleka sadaka elfu 12500

Note: ?Kitu chochote kinachoitwa sadaka kiombee kabla hujakitoa kama siku 2 au 3 ndio uitoe sadaka ?nakama unahitaji kitu mfano Nguo peleka nguo kwa waitaji uone utakavyopata Nguo Nyingi ?chukua mfano Bakhresa na Mengi wanavyojitolea mbona hawaishiwi, siri yao iko kwenye nidhamu hii ya pesa!!

Jaribu na wewe anza hata na kidogo kidogo kuwa na nidhamu na fedha uone nayo itakavyokuheshimu